



duducoelho.com

KOSA LA MAPINDUZI YA KIJANI KWA AFRIKA NI NINI?

Agenda ya Mapinduzi ya Kijani kwa kiasi kikubwa ina ushawishi katika sera za kilimo, programu na uwekezaji katika Afrika. Hii ni dhahiri kutoka kwenye sera ya kanda ya Umoja wa Afrika mpaka kwenye programu za nchi na ushauri unaotolewa na maafisa ugani kwa wakulima.

Ni watu wachache tu kutoka kwenye kundi la wenye uwezo linalofaidika na utaratibu wa Mapinduzi ya Kijani:

- Wakulima hawawezi kuziendea teknolojia za Mapinduzi ya Kijani, kama vile mbegu zilizoboreshwa na kemikali za kilimo, kwasababu ya gharama kubwa.

- Masoko ya kibiashara – pale yanapokuwepo – yanashindwa kunyonya ziada ya mazao yanayozalishwa.
- Wakulima wengi wanashindwa kukidhi vegezo vinavyowekwa vya ujazo, ubora na viwango ili waweze kuuza kwenye masoko makubwa ya kibiashara.
- Bei za bidhaa ni ndogo sana, hasa katika msimu wa mavuno, na wakulima mara chache hutengeneza faida kwa kuuza bidhaa za ziada.
- Kaya zinazolima hubakiza kiasi cha mavuno kwa ajili ya matumizi yao, lakini mara nyingi ni yale yenye ubora hafifu ambayo hupelekea kushuka kwa viwango vya lische.